KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 19, Issue 2
18th Rabiul Awwal 1433
10th Feb, 2012

KUSHEREHEKEA MAZAZI YA MTUME [صلى الله عليه وسلم]

"Wujoob al-Luzoom as-Sunnah wal hadhar minal-Bid'ah" Na: SHEIKH ABDUL AZEEZ BIN ABDULLAAH BIN BAAZ

Sifa zote njema ni Zake Allaah Alietukamilishia dini yetu, na Akatubariki sisi na kutuchagulia Uislamu kuwa ndiyo dini yetu. Swala na salamu zimshukie mtumwa Wake na Mjumbe, aliewalingania watu wamtwi'i Mola wao na akawahadharisha dhidi ya ufujaji, uzushi, na kufanya ma'asia; Tunamuomba Allaah Awabariki ahli zake, maswahaba zake, na wote walofuata nyayo zake hadi siku ya malipo.

Nimepashwa habari mimi kuhusu makala yaliyochapishwa kwenye ukurasa wa kwanza wa jarida la wiki, "Weekly magazine Edarat of Kanpur", lenye makao yake katika mji wa kiufundi wa Uttar Pardesh huko India. Katika makala hayo palikuwemo na maneno ya uchochezi dhidi ya utawala wa kifalme wa Saudi Arabia kuhusu kujiambatanisha kwao na imani iliyo thabiti ya Uislamu na upinzani wake dhidi ya mambo ya uzushi. Muandishi huyo akadai yakuwa imani ya Salaf (Watangulizi wetu wema katika Uislamu), inayoshikiliwa na inayolindwa na ufalme wa ki-Saudi haulingani na Sunnah. Kwa madai hayo, muandishi amekusudia kuzua mgawanyiko baina ya Ahlus-Sunnah na kuhimiza mambo ya uzushi na itikadi mbovu. Tabia hii, hapana shaka ni ya kuchukiza mno na hatari. Nia na malengo yake makubwa ni kuishambulia dini ya Uislamu, na kueneza mambo ya uzushi na upotofu kwenye njia ya haki. Na zaidi ya hapo, makala hayo yalikariri waziwazi mas-ala ya kusherehekea mazazi ya Mtume kama sababu ya kuanzisha mjadala kuhusu imani ya Ufalme na viongozi wake. Kwahivyo, nimeonelea yakuwa ni muhimu kuwapasha watu kuhusu mas-ala haya. Kwa kutaraji usaidizi kutoka kwa Allaah (سبحانه وتعالى), mimi nasema: Hairuhusiwi kusherehekea mazazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) wala ya mtu yoyote. Kwa hakika, ni lazima kuyakemea mambo kama hayo, kwani huwo ni uzushi katika dini. Mtume (صلى الله عليه وسلم) yeye mwenyewe hakuisherehekea wala hakuwaamrisha wengine kumsherehekea yeye. Au kumsherehekea yoyote aliyekufa kabla yake miongoni mwa Mitume, au kuwasherehekea mabinti zake, au wake zake au jamaa zake wengine. Makhalifa waongofu, maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) au wafuasi wao waliowaandama katika haki hawakusherehekea tukio hili, wala yeyote miongoni mwa wanavyuoni wa ki-Islamu katika qarne zilizopita. Wao walikuwa wakizielewa mno Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuliko sisi, walimpenda mno na wakafuata sheria kuwashinda wale walokuja baada yao. Lau kama kusherehekea mazazi yake ingelikuwa ni amali njema, basi na wao wangelitutangulia katika jambo hilo.

Sisi tumeamrishwa kuandama (kufuata) na tukakatazwa kuzua. Hii ni kwa sababu ukamilifu wa dini ya Uislamu na utoshelezaji wa yale tuliyopewa na Allaah na Mtume wake umekubaliwa na Ahlus-Sunnah wal Jamaa'ah, jum'iyyah ya Waislamu ya Maswahaba na wafuasi wao wema. Imepokewa kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yakwamba alisema: ***"Mwenye kuzua kitu kisichokuwemo katika jambo letu hili, atakataliwa nalo."*** [Imepokewa na Bukhaaree na Muslim]. Na kulingana na riwaya ya Muslim, akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): ***"Mwenye kufanya amali isiyokubaliana na jambo letu hili atakataliwa nalo."***

Na katika riwaya nyengine, Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: ***"Shikamaneni na Sunnah zangu na Sunnah za Makhalifa wangu walio katika uongofu. Jiambatisheni nayo (sunnah hizo) na muishikilie madhubuti kwa magego. Na jitahadharini na mambo mapya yanayozuliwa, kwani kila jipya linalozuliwa ni bid'ah na kila bid'ah ni upotofu."***

Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema katika khutbah zake za ijumaa: ***"Kwa hakika maneno yalio ya kweli kabisa ni yale ya Kitabu cha Allaah (Qur'aan) na uongofu ulio bora zaidi ni ule wa Muhammad*** (صلى الله عليه وسلم)***. Na maovu yalio mabaya zaidi ni mambo ya kuzua (yalio mageni katika mafundisho ya Uislamu), na kila jambo lilozuliwa (katika Dini) ni Bid'ah, na kila Bid'ah ni Dhalaalah (njia mbaya, upotofu), na kila Dhalaalah mwisho wake ni motoni."***

Kwahivyo hadeeth hizi zina hadhari kali kuhusu mambo ya kuzua na onyo yakwamba kitendo chochote kama hicho ni upotofu wa kumtoa mtu kwenye njia ya sawa. Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaonya watu kuhusiana na uzito wa mambo hayo ya kuzua na matokeo yake mabaya. Kuna ahaadeeth nyingi sana za kuthibitisha hoja hii katika mas-ala haya. Na Allaah (سبحانه وتعالى) akasema (kama ilivyofasiriwa): "**Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho...**" [Soorah Al-Hashr 59:7] Akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): "**Basi wajihadhari wale wanaokaidi amri yake (Sunnah - njia za kisheria, maamrisho, vitendo vya 'ibaadah, matamshi n.k) (miongoni mwa vipote), usije ukawapata msiba au ikawafika adhabu iumizayo.** [Soorah An-Nur 24:63]. Akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): "**Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Allaah.**" [Soorah Al-Ahzaab 33:21] Akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): "**Na wale waliotangulia wakawa wa kwanza**

YALIYOMO
MAZAZI YA MTUIMЄ 1 - 4

katika (Uislamu) - Muhaajireen na Ansaar, na wale waliowafuata kwa mwendo mzuri - Allaah Atawapa radhi, nao wamridhie (Allaah kwa hayo mazuri atakayowapa). [Soorah At -tawbah 9:100]. Akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa):"**Leo nimekukamilishieni dini yenu, na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe dini yenu.** [Soorah Al-Maaidah 5:3].

Aya hii inathibitisha waziwazi yakwamba Allaah Mtukufu ameikamilishia dini huu Ummah wetu na akaubariki. Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) alifariki baada ya kuufikiliza ujumbe wa Allaah kikamilifu pamoja na sheria zake zinazohusiana na maneno na vitendo. Kisha akatia mkazo yakwamba mambo yote yaliyozuliwa na watu na kuingizwa katika dini ya Uislamu ni uzushi na inatupasa kuyakatalia mbali, hata kama wazushi wenyewe waliyazua kwa nia nzuri. Imethubutu yakwamba Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na wafuasi wao wema waliokuja baada yao walikuwa wakiwaonya watu dhidi ya mambo ya kuzua kwani wao (wazushi) kawaida huongeza mambo katika Uislamu na kuzipitisha sheria zisizoruhusiwa na Allaah, sawa na wafanyavyo maadui wa Allaah kama vile Mayahudi na Manasara waliofanya nyongeza katika dini yao na kuzua wasiyoruhusiwa na Allaah. Na zaidi ya hapo, kuyaruhusu mambo ya uzushi katika Uislamu ni kukiri yakwamba Uislamu haukukamilika na una kasoro. Imani kama hiyo, sio kwamba ni mbovu peke yake, bali inakhalifu ayah ifuatayo, (kama ilivyofasiriwa): "**Leo nimekukamilishieni dini yenu** na ahaadeeth za Mtume (صلى الله عليه وسلم) zenye kutuonya dhidi ya mambo ya kuzua. Tunaposherehekea mazazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) au ya watu wengine kila mwaka, ina maana yakwamba Allaah hakuikamilisha dini kwa Ummah huu, na wala Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwafikilizia watu yaliyopasa kufikilizwa kwao kuhusiana na maamrisho ya dini yao, mpaka hivi karibuni walipokuja watu wa baadae walipoanza kuzua katika dini, yale yasoruhusiwa na Allaah, wakidhani yakwamba mambo hayo yatawakurubisha zaidi kwa Allaah. Bila ya shaka hii ni hatari kubwa na ni kama kumlaumu Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم); Haliyakuwa Allaah (سبحانه وتعالى) tayari ameshaikamilisha dini na kutimiza Baraka zake, na Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliufikiliza ujumbe wake waziwazi na akawafundisha Ummah wake kuhusiana na njia zitakazowafikisha peponi na kuwaepusha na moto wa Jahannam. Kulingana na hadeeth swaheeh iliyopokewa na 'Abdullaah bin 'Amr bin Al -Aas (رضي الله عنه), amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): ***"Allaah*** (سبحانه وتعالى) ***hakumtumiliza mjumbe yoyote, isipokuwa alimshurutisha awaongoze watu wake kwenye njia aliyoijua kuwa ni bora, na kuwaonya dhidi ya mambo aliyoyajua kuwa ni maovu."*** [Imepokewa na Imaam Muslim]. Ni jambo linalojulikana sana yakuwa Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) ni mbora wa Mitume wote, wa mwisho na alokuwa mkamilifu zaidi kuwashinda wote kuhusiana na njia aliyokuwa akiwalingania na kuwanasihi watu wake. Lau kama kusherehekea milaad (maulidi) ingelikuwa ni kitendo cha dini kilichochaguliwa na Allaah kwa watumwa Wake, basi Mtume (صلى الله عليه وسلم) angelikuwa amewaeleza mambo hayo watu wake na wangeliisherehekea wakati wa uhai wake, au Maswahaba zake wangelifanya hivyo. Kwa vile mambo hayo hayakutokea, basi ni wazi yakwamba Uislamu hauna uhusiano wowote na maulidi. Kinyume cha hivyo, jambo hilo ni miongoni mwa mambo ya uzushi ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwatahadharisha nayo watu wake kama tulivyokwisha kutaja hapo awali.

Jamhuri ya wanavyuoni - isitoshe kwamba wameyakataa mambo ya maulidi - lakini wameonya dhidi yake kulingana na ushahidi uliokwisha elezwa hapo mbeleni. Kulingana na hukmu ya kisheria ya ki-Islamu, mas-ala yoyote yanayohusiana na uhalalishaji na mizozo yoyote baina ya watu, ni lazima yapelekwe katika kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) kwa mujibu wa maneno Yake Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyofasiriwa: "**Enyi Mlioamini! Mtiini Allaahna mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Allaahna Mtume, ikiwa mnamwamini Allaahna siku ya mwisho. Hiyo ndiyo kheri, nayo ina matokeo bora kabisa."** [Soorah An-Nisaa 4:59]

Na akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyofasiriwa: "**Na mkikhitalifiana katika jambo lolote (rejeleeni kitabu cha Allaah na hadeeth za Mtume kwani) hukumu yake iko kwa Allaah ."** [Soorah An-Nisaa 4:59]

Katika kuyarudisha mas-ala haya kwenye kitabu cha Allaah, tutaona yakwamba inatupasa sisi kumfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika maamrisho yake na kutukemea dhidi ya kila aliyotukataza. Inazidi kutueleza yakwamba Allaah Amewakamilishia watu dini yao. Kwahivyo maadamu maulidi si miongoni mwa mafunzo ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) hayawezi kuwa ni sehemu ya dini tuliyokamilishiwa na Allaah na akatuamrisha tushikamane nayo kwa kumfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم). Tena tunapolirudisha suala hili kwenye Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم), hatuwakuti Maswahaba wala Mtume mwenyewe, kuwa walikuwa wakifanya jambo hilo au wakiwahimiza wengine wawafanyie. Huu ni ushahidi wa waziwazi yakwamba maulidi si sehemu ya dini, bali ni miongoni mwa mambo ya kuzua na kuwaiga watu wa kitabu (Mayahudi na Manasara) bila ya mazingatio (ki-upofu) kwenye sherehe zao. Tukiuzingatia ugomvi huu, kila moja (alie na uchache wa busara na kuipenda haki na uadilifu), atashuhudia yakwamba kuyasherehekea mazazi ya mtu yoyote hakuhusiani na Uislamu. Bali ni miongoni mwa mambo ya uzushi ambayo Allaah na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) wametoa onyo dhidi yake kwa mkazo. Mtu mwenye busara na asihadaike kwa kuuona Ummah mkubwa wakilifanya jambo hilo kote Ulimwenguni kwa sababu haki inatambuliwa na kujulikana kwa dalili zake za ki-Sheria na wala si kwa vitendo vinavyofanywa na idadi kubwa ya watu. Akasema Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyofasiriwa kuwahusu Mayahudi na Manasara: "**Na walisema: 'Hataingia peponi ila aliye Myahudi au Mkristo.' Hayo ni matamanio yao tu (si hukumu ya Allaah). Sema: 'Leteni dalili zenu, kama nyinyi ni wasema kweli.'** [Soorah Al-Baqarah 2:111]. Na pia akasema tena Allaah (سبحانه وتعالى) kama ilivyofasiriwa: "**Na kama ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Allaah. Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi).** [Soorah Al-An-aam 6:116]

Baadhi kubwa ya haya mambo ya kuzua, juu ya maumbile yake ya ki-uzushi, kawaida hayasalimiki na maovu mengine kama vile mchanganyiko wa mikutano ya wanawake na wanaume, nyimbo zikitumbuizwa kwa vyombo vya miziki, ulevi, madawa ya kulevya, na yanayofanana na hayo. Huenda pia zikahusisha hilo ovu zaidi (nalo ni) la

Shirk kubwa, kwa kuonyesha upindukiaji wa mipaka katika kumtukuza Mtume (صلى الله عليه وسلم) na watu wema wengine na kwa kumuomba yeye, kuomba msaada kutoka kwake, au kuamini yakwamba yeye (Mtume) anayajua yaliyofichamana na madai yote kama hayo yenye kumfanya Mu'min kuwa Mur'tad. Imepokewa hadeeth swaheeh yakwamba amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): ***"Jihadharini na ghuluww (kupindukia mipaka) katika dini, kwani kumewaangamiza waliokuweko kabla yenu."***

Na vilevile akasema (صلى الله عليه وسلم): ***"Musipite kiasi katika kunisifu mimi kama Manasara walivyofanya kwa Issa, mtoto wa Maryam. Mimi ni mtumwa tu. Kwa hivyo kwa urahisi semeni: Mtumwa wa Allaah na Mjumbe Wake."***[Imepokewa na al-Bukhaaree].

Inastaajabisha kuona yakwamba watu wengi sana hujitolea kwa juhudi kubwa kwenye sherehe hizi na kuzitetea kwa vishindo vikubwa; na huku huwaoni kuhudhuria aina fulani za 'ibaadah kama vile swala za kila siku ya ijumaa. Hawana hata haya, wala hawazingatii yakwamba wao wanafanya ma'asia. Bila ya shaka yoyote, hii yaonyesha udhaifu wa imani zao, kuto-ona mbali, na nyoyo zilizojaa kutu kwa ajili ya madhambi na ma'asia. Tunamuomba Allaah (سبحانه وتعالى) Atulinde pamoja na Waislamu wote. Inashangaza kuwaona wengi wao wanaamini yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) huhudhuria maulidi - kuamkuana nae na kumkaribisha. Mbali na kuwa huwo ni urongo usio na msingi, unakuwa ni upumbavu wa hali ya mwisho, kwani Mtume (صلى الله عليه وسلم) hatotoka nje ya kaburi lake kabla ya siku ya kufufuliwa, wala hatokutana na watu au kuhudhuria mikutano yao. Badala yake atabaki mumo humo kaburini hadi siku ya kufufuliwa na roho yake imetulia kwenye kilele cha juu kabisa na Mola Wake katika mahali Patakatifu. Allaah (سبحانه وتعالى) Akasema (kama ilivyofasiriwa): "**Kisha hakika nyinyi baada ya hayo ni wenye kufa. Kisha hakika nyinyi baada ya siku ya Kiama mtafufuliwa.** [Soorah Al-Mu'minun 23:15-16]. Na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): ***"Mimi ndie wa kwanza nitakaefufuliwa kutoka ndani ya kaburi siku ya kufufuliwa na nitakuwa wa kwanza mwenye kuwashufaiya watu na wa kwanza ambae shifa'a yake itakaekubaliwa."*** Ushahidi huo ulokwisha tajwa kutoka kwenye Qur'aan na Hadeeth unathibitisha bila ya shaka yoyote yakwamba waliokufa watatoka makaburini mwao siku ya kufufuliwa peke yake. Wanavyuoni wote wa ki-Islamu wanaafikiana kuhusu jambo hilo. Inampasa kila Muislamu kujua mambo hayo wala asipotoshwe kirahisi na mambo ya bid'ah na ushirikina ulioletwa na watu wajinga wasiokuwa na ruhusa yoyote kutoka kwa Allaah.

Amma kuhusu kumswalia Mtume (kutuma swala na salamu), basi hizo ni katika njia zenye kupendekezwa zaidi na ni amali njema kulingana na maneno yake Allaah (سبحانه وتعالى), (kama ilivyofasiriwa): "**Hakika Allaah anamteremshia rehema Mtume; na Malaika Wake (wanamuombea dua kwa vile vitendo vizuri alivyovifanya). Basi; enyi Waislamu (mliopata neema hii ya kufundishwa haya na Mtume) mswalieni (Mtume, muombeeni rehema) na muombeeni amani.** [Soorah Al-Ahzaab 33:56].

Na akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): ***"Yeyote mwenye kuniswalia mimi mara moja, Allaah Atamswalia yeye mara kumi."***

Imefaridhiwa kila wakati, hususan kila mwisho wa swala. Imefaridhiwa katika tashah-hud ya mwisho ya kila swala na baadhi kubwa ya wanavyuoni. Imetiliwa mkazo mahali pengi, kama vile, pindi baada ya adhaan (muadhini), linapotajwa jina la Mtume (صلى الله عليه وسلم) siku ya ijumaa na usiku kabla yake kulingana na idadi ya ahaadeeth.

Haya ndiyo niliyokusudia kuyafafanua na kuyatilia mkazo kuhusu mas-ala haya. Ni matumaini yangu yakwamba yatamtosheleza kila yule ambae Allaah Aliemuonyesha muangaza. Ni masikitiko yalioje kuwaona Waislamu wenye hima na bidii, wanaojulikana kwa kuwa na Imani imara na mapenzi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakiandaa sherehe kama hizo za uzushi. Na tuwaulize watu kama hao: Hebu tuambieni, ikiwa nyinyi ni miongoni mwa Ahlus-Sunnah na munasema kuwa munamfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم), Jee yeye (Mtume) au yeyote miongoni mwa Maswahaba zake au wale waliowafuata wao waliwahi kufanya mambo hayo, au si chochote zaidi ya kuwaandama ki-upofu maadui wa Uislamu kutoka katika Mayahudi na Manasara na mfano wao? Mapenzi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) hayana mafungamano yoyote na kusherehekea mazazi yake. Kumpenda kihakika ni kwa kumtii, kuyaamini mafunzo yake, kujiepusha na aliyotukataza na kumuabudu Allaah kulingana na alivyotufundisha. Vilevile yanafungamana mambo hayo kwa kumswalia (kumtumia swala na salamu) kila mara, haswa wakati anapotajwa na wakati tunaposwali.

Wahaabiyyah, kulingana na muelekeo wa maelezo ya muandishi huyo, si waanzilishi katika kuupinga uzushi kama huo. Imani yao ni kujiambatanisha na kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم); kuandama nyayo zake na za wafuasi wake waongofu; kuamini na kuyatekeleza yaliyosemwa na watu wema waliotutangulia (ma-Salaf) na ma-Imaam wa ilimu na Uongofu, wenye uwezo wa kutoa hukmu za ki-dini kuhusu 'ilimu ya Allaah, na Sifa Zake za Ukamilifu na Utukufu kama zilivyokwisha kuonyeshwa kwenye kitabu kitakatifu na Ahaadeeth Swaheeh (mafunzo) za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na kama yalivyopokelewa kwa moyo mkunjufu na Maswahaba zake.

Wahaabiyyah wanayaamini mambo hayo kama yalivyopokewa bila ya kuleta mabadiliko, wala kulinganisha na sifa za wana-adamu, kutoa mifano au kuzikataa Sifa hizo. Wameshikilia njia walizokuwanazo Maswahaba na wafuasi wao kutoka katika miongoni mwa wenye ilimu, imani na uchaji Mungu. Wao wanaamini kuwa nguzo kubwa ya imani ni kushuhudia yakwamba hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah. Kwao wao, huu ndiwo mzizi wa imani na ni miongoni mwa kitagaa kikubwa chenye Utukufu.

Wao wanajua kulingana na maafikiano ya Waislamu, yakwamba mzizi huu unahitaji ilimu, kukubali, na kufuata. Inamaanisha yakwamba hapana anaestahiki kuabudiwa isipokuwa Allaah Mtukufu, asie na mshirika kabisa. Inazidi kumaanisha ukanushaji wa ibaada ya kitu chochote kisichokuwa Yeye (Allaah). Inaonyesha sababu ya kuumbwa Majinni na Wana-adamu; kwanini walitumilizwa Mitume na kuteremshwa vitabu. Zaidi ya hayo, 'Ibaadah sio kujisalimisha kikamilifu na kuwa na mapenzi peke yake, bali vilevile ni kutwi'i kikamilifu na kuwa na kicho. Uislamu ndiyo dini ya pekee itokayo kwa Allaah na kusambazwa na Mitume na hakuna chochote, isipokuwa Uislamu, ndiyo dini ikubaliwayo na Allaah ikiwa ni zamani au sasa. Mwenye kujidhalilisha kwa Allaah kwa khiari yake na pia kwa kiumbe mwengine kinyume cha Allaah, huyo ni mushrik (mpagani). Ni sawa na yule anaeswali kwa ajili ya Allaah na kiumbe

mwengine ubavuni Mwake. Amma kwa yule asojidhalilisha Kwake, basi atakuwa anafanya kiburi katika yanayompasa kuyatekeleza kwa Mola wake.
Amesema Allaah (سبحانه وتعالى) (kama ilivyofasiriwa): "**Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila ummah (Jamii, Taifa) ya kwamba (akalinganie watu) "Muabuduni Allaah (Peke Yake) na mwepukeni (Iblisi) muovu."** [Soorah An-Nahl 16:36]
Kwahivyo, Imani ya Wahaabiyyah imeegemezwa juu ya utekelezaji wa ushuhuda yakwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah na kuwachana kabisa na mambo ya uzushi, ushirikina na kila chenye kuhalifu Sheria.
Hii ndiyo Imani aliyokuwa nayo Sheikh Muhammad ibn Abdul-Wahhaab (رحمه الله) na ndiyo aliyowalingania watu. Yeyote mwenye kumzulia chochote kinyume na hayo, mtu huyo juu ya kwamba anasema urongo, pia anafanya madhambi makubwa na anadai mambo yasiyo na ukweli wowote. Hapana shaka yakwamba atayapata yale ambayo Allaah aliyowaahidi kila mwenye kuzua urongo.
Sheikh anaonyesha - kwa kupitia mfululizo wa makala yake mashuhuri na vitabu vya ki -Ilimu kuhusiana na somo la "Udhihirishaji wa Upweke: "*Laa ilaaha illallaah* " - yakwamba hapana apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah (عزّ وجلّ) na kwamba aina hii ya ibaadah isiwe na Shirk ya aina yoyote, si kubwa wala ndogo. Mtu yoyote mwenye kuyafahamu maneno haya anakuwa na urahisi wa kutambua yakwamba mfumo wake hauna tafauti yoyote na ule mfumo walokuwa nao watangulizi wetu wema (Salaf), ma-Imaam wakubwa wenye ilimu na Uongofu. Kwa hakika yeye ameyahuisha yale yote waliyoyafanya maishani mwao kuhusiana na kumuabudu Allaah Peke Yake na kuyatupilia mbali mambo yote ya uzushi na I'tiqadi za ki-Mila. Huu ndiwo msingi wa Dola ya Saudi Arabia na rai hii ndiyo iliyodhihirishwa na Wanavyuoni wa Saudi Arabia. Ujeuri unao-onyeshwa na Serikali ya Saudia unafanyiwa dhidi ya itiqadi za ki-mila na uzushi unaopingana na Uislamu, au aina ya ufujaji wa kupindukia mipaka ambao umepigwa marufuku kabisa na Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم). Waislamu wote, wanavyuoni na viongozi wa Saudi Arabia wanawaheshimu sana na kumpenda kila Muislamu pasi na kujali iwapo amejisajili na kikundi chochote au nchi yoyote Ulimwenguni. Wao wanapinga kila aina ya sherehe au mikutano ya mambo ya uzushi, yasiyokuwa na idhini itokayo kwa Allaah na Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم). Wanayapinga hayo kwa sababu kila jambo jipya katika dini ni uzushi na pia kwa sababu Waislamu wameamrishwa kufuata, na sio kuzua. Uislamu umekamilika na unajitosheleza. Hauhitaji nyongeza yoyote baada ya Allaah na Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) kuyakamilisha maamrisho na Ahlus-Sunnah wal Jamaa'ah, kuanzia kwa Maswahaba, vizazi vyao, na yote yaliyopokewa na wafuasi wao.
Kukataza kusherehekea mazazi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), kutokana na asili yake ya uzushi pamoja na ishara zake za israfu na Shirk inayohusiana nayo kama kawaida, sio ukafiri wala kumdharau Mtume (صلى الله عليه وسلم). Badala yake hicho ni kitendo cha utiifu kwani amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم):

"Jihadharini na ghuluww (kupindukia mipaka) katika mas-ala ya dini. Kwa hakika waliokuwepo kabla yenu waliangamizwa kwa ajili ya kuwa na ghuluww (kupindukia mipaka) katika mas-ala ya dini."

Na akasema tena (صلى الله عليه وسلم):

"Musipite kiasi katika kunisifu mimi kama Manasara walivyofanya kwa Issa, mtoto wa Maryam. Mimi ni mtumwa tu. Kwa hivyo kwa urahisi semeni: Mtumwa wa Allaah na Mjumbe Wake."

Haya ndiyo niliyoyakusudia kuyaeleza kuhusiana na makala hayo yaliyowahi kuchapishwa.
Tunamuomba AllaahAtusaidie pamoja na Waislamu wote tuifahamu Dini Yake; na Azithibitishe nyoyo zetu, tushikamane na Sunnah na tujiepushe na mambo ya uzushi (Bid'ah). Kwa hakika Yeye ni Mkarimu na Mwenye Huruma. Na tunamuomba Allaah Azifikilize Rehma Zake na Baraka Zake juu ya Mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم), Ahli zake, na Maswahaba zake.

JIHADHARI NA BID'AH NA WATU WAKE

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "Yeyote anayezua au akampokea vizuri mzushi (mtu wa bid'ah) basi juu yake laana ya Allah, malaika Wake, na ummah mzima." Ibn Umar (رضي الله عنه) amesema: "Kila jambo la uzushi ni upotofu, hata kama watu wataliona kuwa ni jambo zuri." Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) amesema: "Kwa hakika jambo la kuchukiza zaidi nmbele ya Allah ni mambo ya uzushi." Sufyaan ath-Thawree amesema: "Mambo ya uzushi yanampendeza zaidi Shetani kuliko dhambi, kwani mtu hutubia kutokana na madhambi yake walakin hatubii kwa mambo ya uzushi." Abu Haatim (رحمه الله) amesema: "Alama ya watu wa bid'ah ni kule kupingana kwao na watu wa upokezi wa riwaya." Sufyaan ath-Thawree (رحمه الله) amesema: "Yeyote anayemsikiliza mzushi basi atakuwa ameondoka katika hifadhi ya Allaah na amejiunga na mambo ya uzushi." Ibraheem ibn Maysarah (رحمه الله) amesema: "Yeyote anayemtukuza mzushi basi atakuwa amesaidia katika kuuangamiza Uislamu" Al-Awzaa'ee (رحمه الله) amesema kuwa: 'Umar ibn 'Abdul-'Azeez (رحمه الله) amesema: "Mutakapo ona watu wakikutana kisiri kuhusu mambo ya dini juu ya jambo lolote pasi na kuwahusisha watu wa kawaida – basi jueni yakwaba hao wako katika misingi ya upotofu." Al-Hasan al-Basree (رحمه الله) amesema: Musishiriki katika vikao vya watu wa bida'h (uzushi) na (watu) wenye kufuata matamanio yao, wala musibishane nao, wala musiwasikilize. Al-Fudayl bin 'Iyaadh amesema: Nilikutana na watu walio bora, wote walikuwa ni watu walioshikamana na sunnah na walikuwa wakikataza kuandamana na watu wa bida'h." Imaam Abu Haneefah (رحمه الله) amesema: "Shikamana na hadeeth na njia ya Salaf as-Saalih (watangulizi wema), na jihadhari na mambo mapya yanayozuliwa, kwani yote hayo ni bid'ah." Imaam Malik amesema: "Yeyote anaeanzisha katika Uislamu jambo la uzushi, na akalidhania kuwa ni zuri, basi huyo amedai yakwamba Mtume Muhammad (صلى الله عليه وسلم) amefanya khiyana katika (amana ya kuufikiliza) ujumbe." Amesema tena: "Uovu ulioje walionao watu wazushi, hatuwapi hata salaam!" Imaam ash-Shaafi'ee amesema: "Mtu akutane na Allaah awe amefanya kila aina ya dhambi isipokuwa Shirki tu, ni bora kuliko kukutana na Allaah na ibadah yoyote katika bid'ah." Al-Layth bin Sa'd amesema: "Hata kama lau ningelimuona mtu wa hawaa (matamaniwa – yaani mtu wa bid'ah) atembea juu ya maji, nisingelimkubali." Basi Imaam ash-Shaafi'ee nae akasema: "Yeye (al-Layth) ameteleza kidogo (katika maneno yake). Mimi hata kama ningelimuona atembea angani, nisingelikubali chochote kutoka kwake. Imaam Ahmad amesema: "Katika nguzo muhimu za sunnah kwetu sisi ni: kujiepusha na mambo ya kuzua na kila jambo la uzushi ni upotofu."